KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

THE QUR'AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA

AL-HUDAA [UONGOFU]

الهدى

15/= Ksh

Volume 29

20th Rabi ul-Awwal 1434

1st Feb, 2013

WASILIANA NASI

SIMU (+254) 721473181
Mombasa, Kenya
E-MAIL Info@qssea.net
Web Site: http://www.qssea.net

YALIYOMO KATIKA JARIDA LA WIKI HII

MAANA YA TAWHEED	1 - 3
MACHOZI YA IBN BAAZ	4
MSIMAMO WA AHLU SUN-NAH KUMUHUSU YAZEED	4

HABARI ZA MAZINGIRA YA WAISLAMU KWA MUKHTASAR

Mtu mmoja ameuawa na wengine kujeruhiwa katika shambulizi la kujitoa mhanga nchini Somalia ambapo mshambuliaji amejilipua karibu na ofisi za waziri mkuu

Mlinzi mmoja aliyeshuhudia shambulio hilo alisema kuwa polisi mmoja aliuawa na wengine wawili kujeruhiwa.

Lakini kwa mujibu wa maafisa wa utawala, watu wawili wameuawa na wengine wengi kujeruhiwa katika shambulio hilo lililotokea karibu na makao ya Rais mjni Mogadishu. Mwandishi wa BBC Abdullahi Sheikh mjini Nairobi anasema kuwa maafisa wakuu wanaelezea kuwa lengo la mshambuliaji lilikuwa kulipua ofisi ya waziri mkuu Abdi Farah Shirdon. Lakini wanajeshi waliokuwa wanashika doria walisema walimzuia kufika katika ofisi hiyo. Aidha maafisa walidokeza kwamba mshambuliaji

(Endelea Kwenye Uk. 3)

MAANA YA TAWHEED NA VIGAWANYO VYAKE

NA: ABU AMEENAH BILAL PHILIPS

Maana halisi ya *Tawheed* ni kukipwekesha kitu au kukiita kuwa ni kimoja. Katika lugha ya Kiswahili, kitu kikipwekeshwa huitwa "Pweke". Lakini hata hivyo, kulingana na ufahamu katika Dini ya ki-Islamu maana ya *Tawheed* ni kuamini yakwamba Allaah ndiye Mungu mmoja wa Pekee katika mambo yote tuyafanyayo ili tumridhishe Yeye. Kwa mfano, swala zote zinastahiki kuswaliwa kwa ajili ya Allaah, kuchinja vilevile kunastahiki kutekelezwa kwa jina la Allaah, swadaka na itolewe kwa kumridhisha Allaah na vita vya Jihaad vipiganwe kwa ajili ya Dini ya Allaah Peke yake.

VIGAWANYO VYA TAWHEED

Madda ya Tawheed ina vigawanyo vitatu.

1. *Tawheed ar-Ruboobiyyah:* Upweke katika Uola wake.
2. *Tawheed al-asmaa' was-sifaat:* Upweke katika majina ya Allaah na Sifa zake.
3. *Tawheed al-'Ebaadah:* Upweke katika 'Ibaadah.

1. UPWEKE KATIKA UOLA WAKE

Maana ya *Tawheed ar-Ruboobiyyah* ni kwamba tunamkubali Allaah kuwa Ndiye mtenza nguvu wa kweli katika ulimwengu huu. Yeye ndiye aliyesababisha kila kitu kuwepo haliyakuwa hapakuwa na chochote kabla yake; kwa hiyo, Yeye anaitwa *al-Khaaliq*, Muumba. Yeye ndiye aliyekipa kila kitu nguvu za kukuwa (au kumea), kutembea na kubadilika. Kwahivyo anaitwa *ar-Rabb;* Hapana litokealo isipokuwa analoliruhusu kutokea; kwahiyo, anaitwa al-Maalik, Mfalme wa Ulimwengu huu.

Pindi mtu afanyapo maovu sisi hutambua yakwamba ni Allaah ambaye aliyempa fahamu ya kuyafikiriya maovu hayo, kiwiliwili chenye uwezo wa kutenda maovu hayo, na kwamba halingekuwa jambo ovu isipokuwa kwa idhini ya Allaah akaweza kutekeleza mawazo yake kuyatenda maovu yake aliyoyafikiriya.. Hatufai kusema yakwamba Allaah ndiye aliyemsababisha yeye kufanya mambo maovu, kwa sababu mwana-adamu hujichagulia kufanya

(Endelea kwenye Uk. 2)

MARKAZUL-BAYAAN

MADRASA YA KUHIFADHISHA WATOTO QUR'AN, KATIKA MTAA WA SPARKI, MJINI MOMBASA, INAWATANGAZIA NAFASI ZA KAZI KWA WAALIMU WA KIKE WENYE SHAHADA YA I'DADI NA TAJRIBA KATIKA FANNI YA TAJWEED. KWA MAELEZO ZAIDI, TAFADHALI PIGA SIMU KWENYE MOJAWAPO YA NAMBARI ZIFUATAZO.

0722611034 / 0727458530

(Endelea Kutoka Uk. 1)

maovu yeye peke yake. Badala yake inatupasa kusema yakwamba Allaah alimpa uwezo wa kuweza kufikiriya na kutenda maovu.. Yeye hangeliweza kufanya mambo maovu isipokuwa Allaah aliruhusu kutokea, na hangeliweza kufikiriya kutenda maovu isipokuwa awe amepewa uwezo na Allaah kutekeleza jambo hilo. Lakini yeye mwenyewe alijichagulia kutenda maovu na Allaah akamuacha afanye hayo.

Allaah ndiye mwenye kuendesha kila litokealo, liwapo ni zuri au baya. Sisi tunapotaka kujiepusha na baadhi ya mikasa au kujipatia yaliyo mazuri, inatupasa kumkabili Allaah na kutarajia msaada wake. Lau kama tutakuwa ni wenye kutegemea vitu ambavyo watu wa kawaida wanaviita *talasimu au hirizi* za bahati nzuri (*kama vile miguu ya sungura na kwato za Farasi*) , ili zituletee bahati nzuri, basi tutakuwa tumeuharibu mlango huu wa Tawheed kwa kufanya madhambi makubwa zaidi yanayoweza kufanywa, ambayo ni *Shirk*. Vilevile, iwapo tutakuwa ni wenye kuogopa viumbe wengine ambao watu wa kawaida wanaamini kuwa watasababisha bahati mbaya au nuhusi (*nukhsi*) (*kama vile kumwaga chumvi, paka weusi wapitapo mbele yetu, kuvunja vioo, na kadhaalika*), tukidhani yakwamba tumeziokoa nafsi zetu na *nuhusi* hizi, vilevile tutakuwa tumetekeleza *Shirk* na kujiharibia mlango huu mzima wa Tawheed.

SAMPULI ZA NDONGA ZA SHIRK:

Mguu wa Sungura: Miguu ya nyuma ya Sungura au jozi za dhahabu na fedha za nyayo za nyuma huvaliwa na mamilioni ya watu kwenye nchi za Magharibi kama mkufu au bangili zenye kuleta ishara nzuri. Asili ya Imani hii imetokana na tabia ya Sungura ya kudunda miguu yao ya nyuma kwa mshindo mkubwa katika ardhi. Kulingana na watu wa kale, Sungura huzungumza na roho za walio chini ya ardhi (waliokufa) pindi wanaponyumbuka kwenye ardhi. Kwahiyo, nyayo zao zimehifadhiwa kama njia ya kuufikiliza ujumbe wa matamanio ya mtu kwa roho zilizokufa na pia kama vyombo vya kuleta bahati nzuri kwa ujumla.

KWATO ZA FARASI: Majumba mengi katika bara la Marekani (USA) yana kwato za Farasi zilizogongelewa kwa misumari katika milango yao, mbinu mpya za visanamu vidogo pia huvaliwa kama bangili za hirizi, cheni za funguo au mikufu, kwa imani yakwamba zitaleta bahati nzuri. Asili ya imani hii inaweza kupatikana kutoka kwa visasili vya kale vya ki-Giriki. Katika zama za kale za wa-Giriki, Farasi walizingatiwa kuwa ni wanyama wenye utukufu. Itakapoangikwa kwato ya Farasi kwenye mlango wa mtu, hudhaniwa yakwamba bahati nzuri huja yenyewe. Inalazimu mwishoni mwa kwato ya Farasi palipo wazi paelekezwe juu ili pazuiye hiyo bahati nzuri. Lau sehemu hiyo itaelekea chini, wao huamini yakwamba bahati nzuri yote itamwagika.

KUMWAGA CHUMVI: Imwagwapo chumvi, wengi huamini yakwamba misiba itafuata muda mchache ujao. Kwahiyo, chumvi iliyomwagwa hurushwa juu ya bega la kushoto kwa min-ajil ya kuitaifisha. Asili ya itikadi hii inategemea juu ya uwezo wa chumvi katika kuhifadhi vitu visiharibike. Itikadi hii ndiyo iliyokuwa ya watu wa zamani ifanyike kutokana na nguvu za ki-chawi. Kwahiyo, kumwaga chumvi ikawa ni onyo la mambo mabaya. Kwa-vile, ilidhaniwa yakwamba mashetwani wabaya hukaa kwenye upande wa kushotoni mwa mtu, kurusha chumvi iliyomwagwa juu ya bega la kushoto likawa ni jambo lenye kuwatosheleza mashetwani wabaya.

PAKA WEUSI: Watu wengi wanaamini yakwamba kupitiwa mbele katika njia na Paka mweusi huashiriya kuja kwa bahati mbaya. Itikadi hii ilichimbuka katika miaka ya kati na kati wakati watu walipokuwa wakiamini yakwamba Paka weusi walikuwa ni miongoni mwa wanyama vipenzi wa wachawi. Wachawi waliaminika yakwamba walikuwa wakitengeneza mvinyo wa kichawi kwa mchanganyiko wa ubongo wa Paka mweusi na sehemu ya vyura, nyoka, na vidudu. Atakapoishi Paka mweusi wa mchawi kwa miaka Saba, na asimalizikie kwenye mvinyo, basi Paka huyo atadhaniwa kubadilika na kuwa mchawi.

KUVUNJA KIOO: Wengi wanaamini yakwamba kuvunjika kwa kioo kwa njia ya ajali ni ishara ya miaka saba ya *nuhusi* (bahati mbaya). Watu wa zamani walidhania yakwamba wanapoziona sura zao kwenye maji ndio huwa wameziona roho zao. Kwahivyo sura zao zinapovunjika-vunjika (*kwa mfano*; mtu akitupa kijiwe ndani ya maji), basi roho zao pia zitavunjika-vunjika. Vioo vilipovumbuliwa, itikadi hii pia ilihamishwa kwao.

2. UPWEKE KATIKA MAJINA NA SIFA ZA ALLAAH

Maana ya *Tawheed al-Asmaa' was-Sifaat* ni kumzungumza Allaah kwa njia ya sifa zake kulingana na Majina na Sifa Alizojisifu nazo Yeye mwenyewe katika Qur'an au kwa njia alizotumia Mtume wake Muhammad (صلى الله عليه وسلم) katika kumsifu Yeye. Kwa sababu Allaah ndiye Mtukufu, Majina yake huitwa *al-Asmaa' al-Husnaa* (Majina Mazuri Kabisa). Amesema Allaah katika Qur'an: **"Allaah, hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye. Naye Anayo Majina mazuri."** [Twaa-Haa (20):8].

Viumbe vyote vina Sifa au maumbile ambayo kwayo hujulikana. Sisi tumesoma kwenye somo la sayansi yakwamba wanyama ni tafauti na mimea kutokana na sampuli fulani za ki-maumbile. Wanyama wana uwezo wa kutembea na wengi wao huwaleya watoto wao, haliyakuwa mimea haina sifa kama hizo.

Vilevile, kila Jina la Allaah hueleza aina fulani ya Sifa yenye kumstahiki Yeye peke yake. Kwa mfano, Allaah anajiita Yeye Mwenyewe *al-Awwal,* wa Kwanza, lenye maana yakwamba kabla ya kuwepo kitu chochote, basi Allaah alikuwepo. Hapana kilichokuwepo isipokuwa Allaah, kwa sababu Allaah ameumba kila kitu. Mwanafunzi anaweza kuitwa wa kwanza kwenye darasa au wa kwanza kwenye mashindano, lakini hawezi kuwa ni wa kwanza kabla ya kila kitu. Si Majina ya Allaah wala si Sifa za Allaah zenye kufanana na zile za viumbe vyake. Hatufai kumpa Allaah sifa za viumbe vyake wala hatufai kuwapa viumbe Sifa

(Endelea katika Ukurasa wa 3)

Zake. Amesema Allaah katika Qur'an: **"Hakuna chochote mfano Wake; naye ni Mwenye kusikiya, Mwenye kuona."** [Ash-Shuura (42): 11].

Katika Bibilia ya Makristo na Taurati ya Mayahudi wameandika yakwamba Allaah Ameuumba Ulimwengu kwa siku sita za mwanzo kisha akalala katika siku ya saba. Kwahivyo wao wanachukulia emma siku ya Jumamosi au Jumapili kuwa ni siku ya mapumziko ambayo kufanya kazi kwenye siku hiyo inaonekana kuwa ni *ma'asiya* (madhambi). Hatahivyo, tendo la kumfanya Allaah kuwa ni kama wana-Adamu wenye kuchoka kutokana na kazi wafanyazo mpaka wakawa wanahitaji mapumziko, wamefanya madhambi makubwa ya *Shirk*. Katika Qur'an, Allaah amesema: **"Allaah, hakuna mola ila Yeye, (na) ndiye Mwenye uhai wa maisha, Msimamia kila jambo. Kusinzia hakumshiki wala kulala."** [al-Baqarah (2):255].

3. UPWEKE KATIKA 'IBAADAH

Maana ya *Tawheed al-'Ibaadah* ni kwamba tunaelekeza maombi yetu sote kwa Allaah Peke yake, kwa sababu Yeye ndiye wa Pekee mwenye uwezo wa kuyajibu maombi yetu. Baadhi ya watu husema, "iwapo unataka kumshtakia Mkurugenzi wa mashule, wewe kama mwanafunzi huwezi kwenda wewe mwenyewe kwenye ofisi yake. Itakubidi uzungumze na mwalimu wako ambaye atakayezungumza na mwalimu mkuu, ambaye kwa upande wake, ndiye atakaechukuwa malalamiko yako kwa Mkurugenzi. Katika mfumo kama huo, ni bora kumuuliza mtu aliye karibu na Allaah, kama vile Mitume au watu wema, wakubebee maombi yako. Itikadi kama hiyo humfanya Allaah kuwa kama wana-adamu wenye kuhitaji watu wa kati na kati. Hatahivyo, Allaah ni tafauti, Yeye ni Mwenye kusikiya na ni Mjuzi wa kila kitu, kwahivyo hapana haja ya mtu yoyote kutubebea maombi yetu kwa Allaah". Amesema Allaah katika Qur'an: **"Na Mola wenu anasema: 'Niombeni nitakujibuni."** [Ghaafir (40): 60].

Kwahivyo, kuelekeza maombi yako kwa Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) au watu wengine wema ambao baadhi ya watu wanawaita "*Mawalii*." Wakitumai yakwamba maombi yao yatamfikia Allaah na yatajibiwa kwa kupitia kwao ni *Shirk,* madhambi makubwa kuliko yote.

Inahitaji ibainike yakwamba ibada katika Uislamu inakusanya zaidi ya swala zetu peke yake. Tutakapomfuata mtu mwenye kufanya *halaal* jambo ambalo Allaah alilolifanya kuwa ni *haraam* au kinyume chake, basi tutakuwa pia sisi tunawaabudu wao. Dalili ya hilo inapatikana kwenye hadeeth iliyosimuliwa na 'Adee ibn Haatim yakwamba alimsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisoma aya isemayo: **"Wamewafanya wanavyuoni wao na watawa wao kuwa ni miungu badala ya Allaah."** [at-Tawbah: (9): 31].

Akasema 'Adee ibn Haatim, "Sisi hatukuwa tukiwaabudu wao." Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم) : "*Jee wao hawakuwa wakiyafanya **Haraam** mambo ambayo Allaah aliyoyafanya kuwa ni **halaal** nanyi mukayafanya kuwa ni **haraam,** na wakayafanya **halaal** mambo ambayo Allaah aliyoyafanya kuwa ni **haraam** nanyi mukayafanya kuwa ni **halaal?"*** Akajibu, Na'aam, hakika." kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: "Hiyo ndiyo iliyokuwa 'Ibaada yenu kwao."

(Endelea Kutoka Uk. 1)

alijilipua alipokuwa anahojiwa katika kizuizi kimoja cha polisi karibu na ofisi hiyo. Mshambuliaji alijilipua karibu na ukuta unaotenganisha ubalozi wa Ethiopia na makao ya waziri mkuu. Majengo hayo mawili yako ndani ya eneo ambalo pia linahifadhi makaazi ya rais. Idadi ya washambuliaji wa kujitoa mhanga imekuwa ikipungua tangu wanamgambo wa Al Shabaab kuondoka Mogadishu kuanzia Agosti 2011 lakini hili li dhihirsiho la changamoto inayowakabili maafisa wa usalama katika kupambana na wanamgambo hao. **BBC — LONDON**

MSIMAMO WA AHLUS SUNNAH KUMUHUSU YAZEED, MTOTO WA MU'AAWIYAH

Na: Shaykhul Islaam Taqee ad-Deen ibn Taymiyyah

ASILI: MAJMOO' FATAAWA VOL 3 UK. 130

Kutokana na haya, Imani ya Ahlus Sunnah na wanavyuoni wa Ummah ni kwamba, haifai kumkashifu yeye (Yazeed mtoto wa Mu'aawiyah), wala kupendekezwa.

Saalih, mtoto wa Ahmad bin Hanbal (رحمه الله) amesema, 'Nilimwambia babangu: "Baadhi ya watu wanasema yakwamba wanampenda Yazeed." Akanijibu, "Ewe mwanangu, kuna uwezekano kwa mtu mwenye kumuamini Allaah na siku ya mwisho kuweza kumpenda Yazeed?" Kwahiyo nikasema, "Ewe babangu, basi kwanini humlaani?" Akanijibu, "Ewe kijana changu, wewe ushawahi kumuona babako akimlaani mtu yoyote?"

Vilevile imepokewa kutoka kwake (Imaam Ahmad) yakwamba aliwahi kuambiwa, 'wewe unaandika hadeeth iliyosimuliwa na Yazeed, mtoto wa Mu'aawiyah?"

Nae akajibu, "Laa, tena yeye hathaminiwi (hana sharaf yoyote), kwani sie yeye aliyewafanya watu wa Madinah aliyowafanya?" Kwahivyo, Yazeed, kulingana na wanavyuoni, viongozi wa Waislamu ni Mfalme miongoni mwa wafalme. Wao hawakumpenda kama walivyokuwa wakiwapenda watu wema waliopita, *Mawalii* wa Allaah, na wala hawamkashifu. Hii ni kwa sababu wanavyuoni huwa hawamlaani mtu yoyote aliye Muislamu. Hii ni kutokana na riwaya inayosimulia kuwa mtu mmoja aliyeitwa Hamaar, alikuwa ni mlevi wa kupindukia. Kila anaposhikwa na kuletwa kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akimuadhibu (*yaani; alimuhukumu kulingana na sheriya*). Basi mara mtu mmoja akasema: "Laana ya Allaah imshukie mtu huyu. Sasa ni mara ya ngapi analetwa mbele ya Mtume (صلى الله عليه وسلم)?". Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamjibu: **"Usimlaani, kwa hakika bwana huyu anampenda Allaah na Mtume wake."**

Licha ya hayo, kuna kundi miongoni mwa Ahlus Sunnah wanaoruhusu kumlaani kutokana na imani yao yakwamba amefanya udhalimu kama huo unaomruhusu mtu kumlaani mwenye kutenda.

Wengine wameshikilia rai yakwamba ni lazima apendwe kwa sababu yeye ni Muislamu aliyewahi kuwa mtawala katika zama za Maswahaba nao *walimbay'i* (walikuwa chini ya twa'a yake).

(Endelea katika Uk. 4)

(Endelea kutoka Uk. 3)

Wanasema yakwamba yaliyopokewa kumuhusu yeye si ya kweli, naye alikuwa na mambo fulani mazuri au alijitahidi kadiri ya uwezo wake katika uamuzi wake wa aliyoyatenda. Hatahivyo msimamo wa sawa ni waliyoshikilia ma-Imaam (wanavyuoni wakubwa), yakwamba asifanyiwe *takhsis* (asikusudiwe yeye) ya kupendwa wala asikusudiwe katika kulaaniwa. Pamoja na hayo, iwapo alikuwa ni mtu muharibifu au mtu dhalimu, basi Allaah humsamehe mtu muharibifu na mtu dhalimu, kiasi cha kwamba iwapo mtu huyo ana matendo mazuri aliyoyafanya.
Imepokewa yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم), **"Jeshi la kwanza litakalovamia Mji wa Constantinople litasamehewa."**
Kiongozi wa Jeshi la kwanza lililowahi kuvamia Mji wa Constantinople alikuwa ni Yazeed, mtoto wa Mu'aawiyah; Abu Ayyoob al-Ansaaree (رضي الله عنه) alikuwa pamoja nae... Kwahivyo, ni wajibu kwa mtu kukoma hapo kuhusiana na mas'ala haya, ajiepushe na kumtaja Yazeed bin Mu'aawiyah na kuwatahini Waislamu kuhusiana nae (Yazeed). Kwa hakika huu ni uzushi unaokwenda kinyume na Ahlus Sunnah wal Jamaa'ah. Kutokana na hayo, pote fulani la watu wajinga wanaamini yakwamba Yazeed bin Mu'aawiyah kuwa ni miongoni mwa Maswahaba na kwamba alikuwa ni katika watu wema na katika viongozi waadilifu. Hayo yote ni katika makosa yaliyo dhahiri.

SHEIKH IBN BAAZ: KUMWAGA CHOZI KWA AJILI YA DA'WAH

Na: *Shaykh Ibraheem ibn Aamir ar-Ruhaylee*

Miongoni mwa mifano [*ya tabia nzuri katika kuilingania Dini ya Allaah*] iliyowahi kutajwa kuwahusu baadhi ya wanazuoni wetu, ni yale ambayo yaliyoelezwa kwetu na baadhi ya watu wenye ilimu kumuhusu Sheikh 'Abdul-Azeez Ibn Baaz (رحمه الله). Siku moja alimnaswihi mtu fulani kuhusu mas'ala kadhaa, mtu huyu alikuwa ni mtu mwenye Ilmu tena maarufu sana, lakini alifanya makosa ambayo yaliyosambaa kwa watu wa kawaida; yakawa makosa hayo yamewafikia watu na hususan miongoni mwa wanavyuoni waliokuwa katika nchi yake.
Hatahivyo, huyu mtu akawa ameshupaa juu ya makosa yake hang'atuki nayo. Basi Sheikh Ibn Baaz akamnaswihi na kuendelea kumnaswihi, bila ya kujali huyu mtu hakukubali naswiha hizo zote. Akageuka upande mwengine na kuanza kwenda zake akimuacha Sheikh Ibn Baaz hapohapo, lakini hayo yote hayakumsababisha Sheikh kubadilisha njia zake na hayakumuathiri huruma zake juu yake. Yule mtu alipokurubia kuondoka mahali pale, aligeuka na kumuelekea Sheikh Ibn Baaz, akamuona analia na kubugujikwa na machozi; aliyaona macho ya Sheikh yakimwaga machozi! Hapo ndipo alipomuuliza Sheikh kwanini analia, naye akamjibu: **'Mimi ninashughulishwa tu na hali yako.'**
[Baada ya kusikiya hayo] Yule mtu akawachana na maneno yake na akakubali naswiha kutoka kwa Sh. Ibn Baaz. Hali yake ya kurudi nyuma katika matamshi yake yalitokana na jambo gani? Kutokana na hayo Machozi, machozi hayo ambayo Sheikh aliyoyamwaga kutokana na huruma na ukarimu kwa Waislamu. Allaah ndiye Mwenye kuyaleta kutokana na Rehma Zake. Hii ndiyo sababu mara nyengine, mwenye kuwalingania watu anapokuwa na Rehma kwa Waislamu, Allaah huigeuza [hiyo Rehma] ionekane kwa njia ya machozi. Ndipo yule anayelinganiwa anapo-ona hayo machozi hukubali naswiha. Chozi hilo huwa na athari, na Rehma hiyo ikawa na athari juu ya kurudi nyuma kwa yule anayelinganiwa. Yule mtu hakuathirika kwa dalili na ushahidi, wala hakuathirika kwa ukarimu katika kupambana naye, hatahivyo, ilikuwa ni Huruma na Rehma ambayo Allaah aliyoiweka kwenye nyoyo za Wanavyuoni hao.
[Mas'ala haya mawili] pamoja na naswiha ya kweli kwa Waislamu yana athari, na jambo hili lilitambuliwa na baadhi ya watu. Yaliyotajwa kumuhusu Sheikh Ibn Baaz (رحمه الله) katika ukarimu wake na wenye kuipinga haki, basi hili ni jambo linalojulikana mno na maarufu. Baadhi ya wenye kuipinga haki hupewa majina ya mzaha, na baadhi ya watu pia walikuwa wakitumia majina ya kuwashusha hadhi au matusi dhidi yao. Lakini, Sheikh Ibn Baaz hakuwa akikata tamaa katika kuwalingania kwenye njia ya haki, alikuwa akiwazuru na kudumisha uhusiano nao mpaka hatimae wengi wakaongoka kwa ajili yake. Kutokana na hayo, akawa ndiye Imaam aliyefuatwa kwa wema na katika kuishikilia Sunnah.
Imewahi kusemwa: Sheikh Ibn Baaz anaposema kitu, basi watu huathirika, wakajisalimisha na kuwachana na matamshi yao. Allaah alimuinua Sheikh huyu kwa jambo gani? Kutokana na Huruma zake, naswiha za kweli na Ukarimu wake; na mifano ya alivyokuwa akiamiliana na watu ni mengi. Baadhi ya watu warongo, baadhi ya wenye kuzitaifisha nakala zake (fatawa zake) na darsa zake, baadhi ya wenye kumdharau na kumtweza Sheikh, na pia baadhi ya wenye kutumbukia kwenye makosa - watu wote hao, yeye alikuwa ni mkarimu kwao. Alikuwa akiwapa naswiha viongozi kwa upole, aliyafanya haya mpaka pale Allaah alipompa aliyompa katika mambo mema.